

HALMASHAURI YA MANISPAA YA TEMEKE

(Barua zote zipelekwe kwa Mkurugenzi wa Manispaa ya Temeke)

Tel: +255 22-2928132
Fax: +255 22-2928137
Barua pepe : temekemc@temeke.go.tz
Tovuti: <http://www.temekemc.go.tz>



Ofisi ya Mkurugenzi,
92 Barabara ya Mandela/Taifa
S.L.P 46343,
15883 -DAR ES SALAAM,

Tarehe: 18, Mei, 2017

TANGAZO LA ZABUNI YA UENDESHAJI WA VYOO NDANI YA MANISPAA YA TEMEKE KATIKA KIPINDI CHA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

1. Halmashauri ya Manispaa ya Temeke katika kuboresha ukusanyaji wa mapato yatokanayo na vyoo, imebinafsisha kazi ya uendeshaji wa vyoo kwa kuwatumia wakala wa kukusanya mapato "Revenue Agents" ambao wataingia Mkataba na Halmashauri kuendesha vyoo.
2. Halmashauri ya Manispaa ya Temeke inatangaza zabuni ya uwakala wa uendeshaji wa vyoo kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2017/2018 katika maeneo ya vyoo yafuatayo :-

NAMBA YA ZABUNI	AINA YA ZABUNI	ADA YA ZABUNI KWA KILA	WANAOSTAHILI
LGA/016/2017-18/HQ/NC/01	Uendeshaji wa choo cha Temeke Sterio (Vyoo vitatu)	50,000/=	Makampuni
LGA/016/2017-18/HQ/NC/02	Uendeshaji wa choo soko la Tazara Vetenary (Choo kimoja (1))	50,000/=	Makampuni
LGA/016/2017-18/HQ/NC/03	Uendeshaji wa choo cha Tandika (Choo kimoja (1)).	50,000/=	Makampuni
LGA/016/2017-18/HQ/NC/04	Uendeshaji wa choo cha Mbagala Kampochea (Choo kimoja (1)).	50,000/=	Makampuni
LGA/016/2017-18/HQ/NC/05	Uendeshaji wa choo cha Temeke Sterio (Vyoo vitatu)	50,000/=	Makampuni

3. Halmashauri inakaribisha maombi kutoka kwa kampuni yenye uwezo na uzoefu wa kuendesha vyoo katika maeneo tajwa hapo (2) juu.
4. Masharti na maelekezo ya zabuni.
 - i. Kampuni itakayoomba zabuni iwe imesajiliwa kisheria.
 - ii. Mwombaji aambatishe pamoja na maombi yake nyaraka zifuatazo;
 - Kivuli cha leseni halisi ya biashara.
 - Kivuli cha cheti cha usajili wa mlipa kodi TIN/VAT.
 - Kivuli cha stakabadhi ya ada ya maombi.
 - Mchaganuo wa makusanyo na matumizi.
 - iii Ada ya maombi ni sh **50,000.00** kwa kila ombi ambazo zitalipwa taslim na kupokelewa na karani wa fedha katika ofisi ya Mweka Hazina na kukatiwa stakabadhi.
 - iv Mwombaji anaruhusiwa kuomba choo kimoja moja au zaidi ili mradi alipie ada ya maombi kwa kila choo.
 - v Mwombaji aliyeshinda zabuni atalipa dhamana ya Mkataba ikiwa ni sawa na kiwango cha miezi miwili wakati wa kufunga Mkataba kabla hajaanza kukusanya.
 - vi Maombi yote yatatumia nyaraka za zabuni zinazopatikana kwenye ofisi ya Katibu wa bodi ya zabuni Manispaa ya Temeke baada ya kulipia ada ya maombi.
 - vii Maombi yafungwe vizuri kwenye bahasha na juu yake iandikwe utambulisho wa zabuni “ **Maelezo ya uendeshaji wa choo**” na kutumwa kwa anuani ifuatayo: -

Katibu,
Bodi ya zabuni,
Halmashauri ya Manispaa ya Temeke,
S L P 46343, **Dar es salaam.**
 - viii. Mwombaji aonyeshe mchanganuo wa maoteo ya mapato anayotarajia kukusanya, matumizi anayotarajia kuyafanya na kiasi atakachoilipa Halmashauri kwa kila mwezi.
5. Mwisho wa kutuma maombi ni siku ya **Ijumaa tarehe 02 Juni, 2017** saa 5.00 asubuhi na ufunguzi utafanyika mara baada ya muda wa kupokelewa kuisha mbele ya wawakilishi wa watoa huduma waliochagua kuhudhuria ufunguzi kwenye ukumbi wa mikutano wa PMU uliopo makao makuu ya manispaa ya Temeke.
6. Maombi yote ambayo yatatumwa baada ya muda wa mwisho wa kuwasilisha maombi hayatapokelewa.

Mkurugenzi wa Manispaa
TEMEKE